TUTAFANYA NINI ILI TUIZUIYE?

- **Kuwahamasisha watu** katika serikali, taasisi za meno, wataalamu wa kiafya, walimu na wahisani barani Afrika na katika nchi ambazo watu huamia.
- Kuelimisha **vikundi vya akina mama** kuhusu hatari ya ung'oaji wa meno ya watoto. **Akina baba** nao waelimishwe kwa kuwa hutawala maamuzi mengi nyumbani.
- Kutoa **vifaa vya kufundishia** kulingana na tamaduni katika nchi hizi 'Dentaid' imetoa vijitabu na mabango ikishirikiana na Christian Relief Uganda ili vitumike kuwaelimisha watu vijijini dhidi ya uongo kuhusu 'ebiino'



- **Kuwatia** moyo **waganga wa kienyeji** kwa kusifu kazi zao nzuri na wakati huo huo kusisitiza kwamba haifai kung'oa meno ya watoto wachanga.
- Kuazimia kuzuia homa na kuhara kwa **kuzingatia usafi** wa mwili, nyumba na **maji**.
- Kuendeleza **uchunguzi** kuhusu ueneaji wa IOM katika nchi hizi na zingine.

NITASAIDIAJE?

- Kusaidia Dentaid katika lengo lake la **kuhamazisha watu** kuhusu IOM. Nakala za karatasi hii zinapatikana kutoka Dentaid.
- Kutoa **msaada** kwa Dentaid ili iweze kutengeneza vifaa vya kuelimisha watu na vipindi vya kupiga vita ung'oaji meno bandia.
- **Kutoa habari** kwa Dentaid kuhusu uwepo wa ung'oaji wa meno bandia (IOM) katika nchi yoyote.

Kwa habari zaidi kuhusu **(IOM)** soma tovuti na uchanganuzi mwingine wa makala kuhusu swala hili kutoka
www.dentaid.org/whatwedo/iommaterials

dentaid
KUBORESHA AFYA YA MENO DUNIANI

Giles Lane, Landford
Salisbury, Wiltshire, UK
SP5 2BG

Tel: +44 1794 324249

Kwa habari zaidi, wasiliana kwa info@dentaid.org

www.dentaid.org

Registered Charity No: 1075826

© Dentaid 2012

dentaid
KUBORESHA AFYA YA MENO DUNIANI

Hatua dhidi ya

KUNG'OLEWA KWA MENO YA MTOTO MCHANGA

KUNG'OLEWA KWA MENO YA WATOTO WACHANGA (IOM) NI NINI?

Neno hili **(IOM)** ina asili ya ulaya linalotumika kurejelea upasuaji wa kienyeji uliofanywa hasa na waganga, makuhani na wakunga kama tiba iliyokubalika kwa magonjwa kinywani mwa watoto wachanga. Katika nchi za Afrika mashariki, inajulikana kwa majina kama vile 'ebiino' huko Uganda ama 'nylon/meno ya plastiki au meno bandia' nchini Tanzania na Kenya.

Watoto wachanga wenye dalili ya kuhara au kuharisha na au kuwa na joto mwilini (homa) hutibiwa kwa kung'olewa kwa meno yaliyovimbisha ufizi kwa fikra kuwa yana viini vya maradhi.

UPASUAJI UNAFANYWAJE?

Sehemu yenye uvimbe hukatwa kwa vyombo visivyo safi na vinavyosababisha uchungu. Vyombo hivyo ni kama waya wa gurudumu la baisikeli, msumari moto, kijisu na kadhalika.

MATOKEO YAKE NINI?

Umwagaji wa damu na mshtuko kutokana na hali ya upasuaji ambao husababisha anemia. Mbinu hizi za upasuaji hazina usafi hivyo husababisha maradhi yanayotokana na damu chafu, tetenasi (pepopunda), kuambukizwa magonjwa yanayohusiana na utokaji wa damu kama vile ukimwi. Mara nyingine husababisha vifo. Madhara ya baadaye hujumuisha kuharibiwa au kuondolewa kwa sehemu muhimu zinazohusiana na ukuaji wa meno mtoto.

Mtoto huyu alifariki kutokana na uchafuzi wa damu baada ya meno yake kung'olewa na mganga wa kijiji kwa kutumia waya uliionolewa wa gurudumu la baiskeli.

UPASUAJI HUU HUFANYIKA WAPI?



Hata hivyo ripoti mbalimbali zasema kuwa upasuaji huu (IOM) umeonekana kwa wahamiaji kutoka nchi hizo hapo juu waliokwenda Israeli, Ufaransa, Marekani, Austrelia, Norway na ulaya. Hili laonyesha haja ya kuwa na wataalamu wa meno katika nchi zilizoimarika kiuchumi kutahadhari ili kutambua matokeo ya upasuaji huu kwa wagonjwa wao.

TUTALITAMBUAJE?

Dalili inayoonekana sana ni ukosefu wa meno ya watoto. Tanzania na Uganda zina visa asilimia 95 vya ung'oaji wa meno bandia ya watoto wachanga. Ung'oajihuonekana hasa kwenye taya ya chini mara tatu zaidi kuliko taya ya juu. Aghalabu uvimbe unaosababisha na kuanza kuota kwa meno huonekana kwa urahisi taya ya chini.

Mtoto kutoka Uganda anayekosa meno yake ya kwanza.

Meno yaliyobadilika umbo ni dalili nyingine kuwa meno ya kwanza yanapong'olewa, yatakayo ota baadaye yataathirika.

WANAOAMINI HAYA NI AKINA NANI?

- **Mganga wa kienyeji;-** Ni mtu asiye na elimu ya udaktari lakini watu katika jamii humwamini kama mtu anayeweza kutibu au kutoa huduma ya kiafya

- **Watu katika maeneo** haya wanaamini kabisa kazi za waganga ambao hutembelewa kwanza hata kama kuna mahali pa kupata tiba ya kisasa.

- **Wasomi** kama vile walimu na wajuzi wa meno wanaosemekana kuamini kuwepo kwa meno bandia yanayohitaji kung'olewa.

UKUUAJI WA MENO: UWONGO NA UKWELI

Kuna uwongo hatari unaodai kuwa kuna uhusiano baina ya dalili (kama vile homa au joto mwilini na kuhara au kuharisha) na ukuaji au kuota kwa meno ya mtoto mchanga umekuwa kwa miaka mingi sasa.

Ukweli: Uchunguzi wa madaktari haujapata ukuaji wa meno ya watoto kusababisha homa, maambukizo au kuharisha.

Ukweli: Kuamini haya kunasababisha kucheleweshwa kwa ugunduzi na matibabu ya maradhi ambayo wakati mwingine husababisha maafa.

Ukweli: Uchunguzi wa kisasa wa madaktari unaonyesha kuwa kuota kwa meno ya watoto husababisha maumivu madogo, kukosa utulivu, kutokwa kwa mate kinywani, kunyonya vidole, kukosa hamu ya chakula na wakati mwingine kukosekana kwa dalili zozote.

Funzo: Mtoto aliye na homa (joto mwilini), anayehara (kuharisha) au mgonjwa anahitaji huduma ya daktari.

Kuota kwa meno hakusababishi haya.